



## **MAMLUKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI ZANZIBAR**

**S.L.P. 3650**

**VICTORIA GARDEN  
ZANZIBAR**

**SIMU: 024 223 2916**

**MOB: 0774 824242**

**FAX: 024 223 1461**

---

MAHAKAMA Kuu Vuga imewaamuru washtakiwa watatu kurudisha kiasi cha shilingi Milioni Ishirini na Tatu Laki Nne Khamsini na Saba Elfu na Mia Mbili (23,457,200) fedha ambazo ziliibiwa kutoka Serikalini.

Mbali ya kurudisha fedha hizo Mahakama hiyo pia imewaamuru washtakiwa hao kulipa faini ya shilingi Milioni Kumi na Tano (15,000,000) ambapo kwa kila mshtakiwa alitakiwa kulipa faini ya shilingi Milioni Tano ili kuwa fundisho kwao na watu wengine wenye tabia kama hiyo, adhabu hizo ni kwa mujibu wa kifungu namba 61 cha Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar na kifungu cha 8(a) cha sheria ya Kuzuia Utakatishaji wa Fedha Haramu.

Washtakiwa hao ni Rahma Suleiman Maalim (36) mkaazi wa Kibweni wilaya ya Magharibi 'A' Unguja, Zainab Abdallah Amour (50) mkaazi wa Kijitoupele wilaya ya Maghjribi 'B' Unguja ambao hao ni wafanyakazi kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Salum Chande Ussi (42) mkaazi wa Tomondo Wilaya ya Magharibi 'B' Unguja ambaye yeye si mtumishi wa Serikali lakini alighushiwa kuwa ndio mnufaika wa mafao hayo.

Washtakiwa hao kwa pamoja walishitakiwa Mahakamani hapo kwa makosa matano tofauti.

Jaji wa Mahakama hiyo Haji Omar Haji, alitoa adhabu hiyo baada ya washtakiwa hao kusomewa mashtaka yao na kukubali, hatua ambayo ilimfanya Jaji huyo kuwaona watu hao ni wakosa kwa mujibu wa Sheria.

Miongoni mwa makosa yaliyokuwa yakiwakabili washtakiwa hao ni pamoja na matumizi mabaya ya mali za Serikali kinyume na kifungu 42(1), (a), (3) na kifungu cha 53 cha Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar namba moja ya mwaka 2012.

Akisoma hukumu hiyo Jaji huyo alisema washtakiwa hao wote kwa pamoja mnamo mwezi wa Juni mwaka 2016 katika maeneo tofauti ya Vuga Wilaya ya Mjini Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, walifanya kitendo cha kuvunja Sheria na kwa njia ya udanganyifu waliweza kujipatia fedha za kitanzania shilingi Milioni Ishirini na Tatu Laki Nne Khamsini na Saba Elfu na Mia Mbili (23,457,200), fedha ambazo ni mali ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Kosa la pili ni utakatishaji wa fedha haramu kinyume na kifungu cha 49 cha Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar kikisomeka sambamba na kifungu cha 7(1), (2), (a) cha sheria ya Kuzuia Utakatishaji wa Fedha Haramu Sheria namba 10 ya mwaka 2009 kama ilivyofanyiwa marekebisho.

Hata hivyo aliendelea kufahamisha kwamba kosa la tatu ni kughushi kinyume na kifungu cha 340(a) na (342) cha Sheria ya Adhabu namba 6 ya mwaka 2004 Sheria ya Zanzibar.

Hati hiyo ilieleza kwamba washitakiwa hao wote kwa pamoja mnamo Juni 2 ya mwaka 2016 katika maeneo ya Maisara Wilaya ya Mjini Unguja walifanikiwa

kutengeneza nyaraka ya uongo kwa lengo la kupata kiinua mgongo ambacho hawakustahiki kitendo ambacho nikosa kwa mujibu wa Sheria.

Sambamba na hayo ilieleza kosa la nne ni kutengeneza nyaraka za uongo kinyume na kifungu 344 cha Sheria ya Adhabu namba 6 ya mwaka 2004 wote kwa pamoja mnamo Juni 2 ya mwaka 2016 kwa kujua na kufanya udanganyifu walitengeneza nyaraka za uongo ili wapate kiinua mgongo hewa.

Kosa la tano ni kutengeneza nyaraka za uongo kinyume na kifungu cha 344 cha sheria ya adhabu namba 6 ya mwaka 2004 sheria ya Zanzibar Washitakiwa hao wote kwa pamoja mnamo Oktoba 10, 2016, huko Vuga Wilaya ya Mjini Unguja kwa kujua na kwa njia ya udanganyifu walitengeneza nyaraka ya uongo ya Serikali ili wajipatie kiinua mgongo kutoka Wizara ya Fedha Zanzibar, huku wakijua kitendo hicho ni kosa kisheria.

Kesi hiyo ilifunguliwa Mahakamani hapo May 10 mwaka 2021, na washitakiwa hao kwa pamoja baada ya kusomewa shitaka hilo walikubali na ndipo mahakama hiyo ilipowaamuru kulipa fedha hizo ili kuwa fundisho kwao na wengine wenyetabia kama hiyo.

Waendesha mashitaka kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka (DPP), Mohammed Haji Kombo, Nassor Z. Mohamed na Nasra Khamis Said, baada ya kusikiliza maelezo kutoka kwa Wakili wa washitakiwa hao waliiomba Mahakama hiyo kutoa adhabu kwa mujibu wa sheria ili kuwa fundisho kwao na watu wengine wenyetabia kama hizo.

Washitakiwa hao kwa pamoja walifanikiwa kulipa fedha hizo.